Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

*HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA*

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# CHAPISHO NA. 6

## DESTURI NZURI KATIKA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI

## KUJIFUNZA KUTOKA KATIKA KANDA

**MASUALA MUHIMU:**

- Pote mashariki na kusini mwa Afrika wanyampori ni raslimali muhimu , lakini nchi zingine zimekuwa na desturi zenye usimamizi wenye tija kuliko nchi zingine.
- Nchini Kenya, wanyama wamepungua kwa asilimia 50 tangu katikati ya miaka ya 1970, kwa sababu katazo la uwindaji wa mwaka 1977 inapunguza chaguzi za kiuchumi kwa serikali, jamii na watu binafsi kutokana na wanyamapori. Ambako biashara imara za utalii wa picha zina msingi mzuri na kuzalisha mapato kwa wenye ardhi, wanyamapori Kenya wameongezeka au kuendelea sawa mathalani Wilaya za Kajiado na Laikipia.
- Namibia ina moja ya mifumo yenye mafanikio mazuri ya usimamizi wa wanyamapori katika Afrika, ambako wanyamapori wanaongezeka, thamani ya wanyamapori kitaifa inaendelea kukua, na mapato zaidi ya jamii yanatokana na wanyamapori. Umuhimu wa mfumo wa Namibia ni kwamba wanajamii na wenye ardhi binafsi wana mamlaka ya kufaidika kwa asilimia 100 ya mapato ya wanyamapori katika ardhi zao.
- Somo la msingi kutoka kwa uzoefu na usimamizi wa wanyamapori wa kanda ni kwamba nchi zilizowezesha watu binafsi wa jamii na umoja wa wenye ardhi ili kufaidika na thamani kiuchumi ya wanyamapori, zinaweza kukuza idadi ya wanyamapori na kuongeza mapato kijamii na kitaifa kutokana na wanyamapori.

*Kwa kushirikiana na*

policy forum · WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY · WWF · PINGO's FORUM

*© JMT 2008*

## Kuendeleza mafanikio na kujumuisha uzoefu wa kanda

Nchi zingine katika kanda zina uzoefu na somo la maana kwa Tanzania kuhusiana na desturi bora na njia bunifu za kukuza mapato ya matumizi ya wanyamapori  - kiuchumi, kiikolojia na kijamii.

Kwa ujumla, nchi kusini mwa Afika kama vile Namibia, Botswana, Zimbabwe, na Afrika Kusini zina uwezo wa kusimamia wanyamapori hadi idadi ya wanyama wa spishi nyingi imetulia sawa au kukua, na mafao kutokana na wanyamapori katika ngazi za jamii na Taifa yameongezeka sana.

*Kielelezo Na. I:  Mwenendo wa idadi ya Faru weusi nchini Namibia na Afrika ya Kusini, I980-2004, Maeneo Tengefu*




*Chanzo:  Nelson 2006*

*Kwa mfano*:

- ➩  Afrika Kusini na Namibia pamoja zina theluthi moja ya vifaru weusi Afrika (angalia Kielelezo Na. 1), kwa sababu idadi ya faru imeongezeka miaka 20 mfululizo wakati idadi ya faru katika nchi kama Tanzania na Zambia ikiwa inapungua sana tangu miaka ya 1970.
- ➩  Mashariki mwa Afrika sera na matendo kwa wanyamapori zina mafanikio machache zaidi. Ingawa mapato kiuchumi ya kutokanana utalii yameongezeka, idadi ya wanyamapori imepungua ilivyoelezewa katika Chapisho Na. 1. Idadi ya wanyamapori Kenya imepungua zaidi hata kuliko Tanzania.

Kwa hiyo chapisho hili linatoa muhtasari wa matokeo ya usimamizi nchini Kenya na Namibia ili kutoa mwanga wa masomo makuu kwa watungaji sera wa Tanzania.

## Kenya
## Wingu jeusi lenye ukanda wa fedha

Kihistoria, Kenya imekuwa na umaarufu wa kimataifa barani Afrika kwa wanyamapori na utalii wa wanyamapori. Lakini Kenya imepoteza wanyama wake wengi na sasa inakabiliwa na changamoto za kiuhifadhi na kiusimamizi kuliko Tanzania. Serikali ya Kenya imekusanya takwimu nzuri juu ya idadi ya wanyamapori tangu miaka ya 1970 na takwimu hizo zinaonesha kuwa spishi nyingi za wanyama zimepungua kwa takriban asilimia 40 kuanzia katikati ya miaka 1970 hadi katikati ya miaka 1990 (Kielelezo Na. 2). Wanyamapori wameendelea kupotea katika sehemu nyingi tangu miaka ya 1990 na **leo Kenya inakadiriwa kuwa imepoteza karibu nusu ya idadi ya wanyama wote kwa kipindi cha miaka 30 iliopita**.

Tofauti na Tanzania Kenya imezuia ukiwemo uwindaji wa kiutalii katika mwaka 1977. Hii ilikuwa na lengo la kulinda wanyamapori, **lakini takwimu zinadhihirisha kuwa sera ya Kenya ya kuzuia uwindaji imeshindwa.** Sababu kuu ya kupungua wa wanyama kwa kipindi kirefu ni kwamba idadi ya watu imeongezeka nchini Kenya na shinikizo dhidi ya ardhi na raslimali limeongezeka. Na kutokana na kuzuia uwindaji, wanyamapori wamekosa thamani ya kiuchumi hasa maeneo ambayo yako mbali kwa utalii wa kupiga picha kama vile kaskazini mwa Kenya.

Thamani pekee ya wanyamapori katika maeneo haya ni nyama inayowindwa kwa njia ya haramu, na hii imekuwa ni biashara nzuri lakini yenye uharibifu inayochangia kupungua kwa idadi ya wanyamapori.

> ***Katika <u>Tanzania</u> tatizo sugu linalokabili uhifadhi wa wanyamapori ni kwamba katika ardhi za vijiji wanyamapori hawana thamani ya kiuchumi kwa jamii, kwa sababu karibu mapato yote kutoka uvunaji wanyamapori (uwindaji wa kiutalii) huenda serikalini.***
>
> ***Nchini <u>Kenya</u> mzizi wa tatizo ni kwamba hakuna mapato kutoka uwindaji wa kiutalii kabisa!***
>
> ***<u>Lakini matokeo yanafanana</u>: Wanyamapori si matumizi yenye thamani ya ardhi katika ngazi ya kijiji, na hivyo wanyamapori hupungua na kutoweka.***

*Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa idadi ya Wanyamapori Kenya, 1970-1990*




*Chanzo: DRSRS 1996;Western et al 2006*

Kwa vile wanyamapori wamekuwa na thamani ndogo au kukosa thamani kisheria kwa wanajamii na watu wenye ardhi binafsi nchini Kenya, wanyama hawajalindwa na wamepungua.

**Muhimu, mwenendo wa wanyamapori nchini Kenya umetofautiana katika maeneo machache, ambako utalii wa picha umeleta <u>fursa za kiuchumi</u> kutegemeana na wanyamapori.**

Idadi ya wanyama haijabadilika wilayani Kajiado na imeongezeka katika Wilaya ya Laikipia kwa kipindi cha miaka 20 iliyopita.

*Kwa mfano*:

⇨ Idadi ya pundamilia huku Laikipia iliongezeka kutoka wanyama 6000 mwisho mwa miaka ya 1960 hadi zaidi ya 30,000 mwaka 1990. Wanyama walao nyama kama vile simba na fisi wameendelea an mtawanyiko mzuri katika maeneo haya, na wanyama walio hatarini kama mbwa mwitu walirejea Laikipia mwaka 2000, na kuongezeka kwa kasi kwa miaka nane iliyopita.

⇨ Maeneo ya wanyamapori wilayani Laikipia yote ni ya binafsi na ya ardhi za vijiji (nchini Kenya maeneo haya ya kiufugaji ya vijiji yanaitwa 'ranchi za makundi'), na ni katika maeneo haya wanyama wamerejea na kuongezeka.

⇨ Laikipia imeandaa biashara kabambe ya utalii wa wanyamapori na hii ndiyo imesababisha ongezeko la wanyamapori, na ranchi binafsi na jamii wanatenga maeneo ya kuhifadhi wanyamapori kwa sababu ya manufaa yao.

⇨ Vilevile Kajiado wanajamii (makundi ya ranchi) wana mikataba ya makubaliano ya kiutalii ambayo imesababisha jamii kutenga ardhi kwa ajili ya wanyamapori ambayo hutumia muda mrefu katika ardhi ya ranchi nje ya Hifadhi ya Amboseli.

## Namibia – sekta ya wanyamapori iliyopinduliwa na kufaidisha kila mmoja

Namibia ina rekodi imara yamafanikio katika kuhifadhi na kurejesha idadi ya wanyamapori na kupanua manufaa ya kiuchumi kutokana na wanyamapori. Katikati ya miaka 1960 Namibia iliwapa wamiliki binafsi wa ardhi haki za kutumia na kusimamia wanyamapori katika ranchi zao. Hii ilisababishwa ongezeko la wanyamapori kwa asilimia 80 katika ardhi binafsi kuanzia miaka ya 1970 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990.

*Kielelezo Na. 3: Kadirio la idadi ya wanyama wanavyoongezeka katika ardhi za jamii kaskazini-magharibi mwa Namibia, 1998 hadi 2006*




*Chanzo: Weaver & Skyer 2005*

Katikati ya miaka ya 1990, baada ya uhuru kutoka Afrika ya Kusini, Namibia ilibadilisha sheria zake za wanyamapori ili kuruhusu jamii kuanzisha maeneo ya hifadhi ambako watapewa haki ya kutumia na kumiliki wanyamapori.

Kuanzi 1998, wakati hifadhi ya jamii ya kwanza ilianzishwa, maeneo 50 ya hifadhi za jamii sasa yameanzishwa yakichukua eneo la kilomita za mraba 120,000 ya ardhi sawa na asilimia 14 ya eneo la ardhi ya Namibia. Hii imerudisha wanyamapori wengi katika ardhi za jamii nchini Namibia (Kielelezo Na. 3). Spishi za kawaida kama vile jamii ya swala na pundamilia zimeongezeka katika maeneo ya jamii Namibia kama ilivyo kwa spishi adimu kama vile faru weusi.

Hifadhi za jamii kaskazini-magharibi mwa Namibia zina idadi kubwa ya faru weusi katika Afrika ambao hawako ndani ya uzio, nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na serikali duniani.

*Kielelezo Na. 4: Kuongezeka pato kwa Hifadhi za Kijamii Namibia, 1998-2006*




*Chanzo: NASCO 2006*

Wanyamapori wamerejea katika ardhi binafsi na ardhi za jamii kwa sababu ya kuwapa uthibiti wa kisheria wa kusimamia wanyamapori na manufaa ya kiuchumi kutokana na wanyamapori. Hii huwapa sababu ya kuhifadhi wanyamapori na kukubali kuwa wanyamapori ni moja ya matumizi muhimu ya ardhi.

Kipengele cha muhimu kisheria kinachosimamia uhifadhi wa jamii nchini Namibia ni kuwa jamii hubakiza asilimia 100 ya mapato yatokanayo na wanyamapori katika maeneo yao. Hii inafanya wanyamapori wawe na ushindani mkubwa kama moja ya matumizi ya ardhi na inatoa motisha kubwa kwa jamii kuhifadhi wanyamapori.

Tangu 1998 wakati jamii karibu hazikupata mapato kutokana na wanyamapori, mapato kutokana na maeneo ya hifadhi jamii yameongezeka sana na sasa yamefikia takriban dola za kimarekani 2.5 million (TZS bilioni 3) kwa mwaka katika hifadhi za jamii 50 (Kielelezo Na. 4). Hii ina wastani wa dola za kimarekani 50,000 (TZS milioni 69) kwa kila hifadhi jamii kwa mwaka, ingawa baadhi ya hifadhi jamii mpya hazijaanza kupata mapato ya kutosha na **zingine zimejijenga na zinapata zaidi ya dola za kimarekani 100,000 (TZS milioni 120 million) kwa mwaka.**
**Je, ni vijiji vingapi Tanzania vinapata kiasi kama hicho kutokana na wanyamapori walio katika ardhi za vijiji?**

Biashara ya utalii imepanuka sana, kama ambavyo wanyamapori wamerejea katika maeneo ya vijiji. Na hii pia inafanya Hifadhi za Taifa za Namibia ziweendelevu zaidi kwa sababu wanyamapori wamehifadhiwa kote, katika maeneo ya serikali, maeneo binafsi na maeneo ya jamii.

***Wakati jamii wanafaidika kwa asilimia 100 kutokana na mapato ya wanyamapori mfumo wa Namia unaunda ukuaji wa uchumi kitaifa kupitia kwa ukuaji wa biashara ya utalii - kama vile kupanua msingi wa kodi, kuongeza mapato ya fedha za kigeni, kuongezeka pato la ndani la kitaia na kuongeza ajira.***

***Kuongezeka kwa idadi na spishi za wanyamapori ambao wanaweza kuvunwa huongeza mapato ya kiuchumi kutokana na wanyamapori nchini Namibia, lakini cha muhimu kwa mapato yote ni kuwapa jamii haki za kupata mafao ya moja kwa moja kutokana na wanyamapori katika ardhi zao. Hivyo, kwa kuwapa wamiliki haki za kutumia wanyamapori, serikali inaongeza mapato kutokana na kodi katika biashara ya wanyamapori na huongeza thamani ya wanyamapori kwa uchumi wa Taifa.***

***Somo muhimu katika uzoefu huo wa kikanda juu ya usimamizi wa wanyamapori ni kwamba nchi ambazo zimewezesha watu binafsi na wanajamii kupata thamani ya kiuchumi ya wanyamapori zimeweza kuongeza idadi ya wanyamapori na pia kuongeza mafao katika jamii na Taifa kutokana na wanyamapori.***

*Kielelezo Na. 5: Kuongezeka kwa idadi ya wanyama wa kuwindwa nchini Namibia, ikiwa ni matokeo ya ongezeko la idadi ya wanyamapori katika ardhi binafsi na ardhi ya jamii 1994-2004*




*Chanzo: DAMM African Indaba*

Kwa sababu idadi ya wanyamapori inaongezeka, Namibia inaweza kuwavuna wanyama wengi zaidi kila mwaka na kiasi cha wanyama wa kuwindwa kimeongezekwa zaidi kwa muongo uliopita (Kielelezo Na. 5).
Nchi ambazo hazijafanya hili, au zilizozuia uwindaji kama vile Kenya, zimeweka mazingira ambayo wanyama hawathaminiki na mwananchi wa kawaida na matokeo yake, wanyamapori wanapungua. Kwa sasa Tanzania wanajamii wanaendelea kupata faida kidogo kutokana na wanyamapori na idadi ya wanyamapori inaendelea kupungua, kama ilivyoelezwa katika Machapisho Na. 1 and 2.